

# MAJIBU YA KISWAHILI

## **SALAMU**

- |             |             |          |
|-------------|-------------|----------|
| 1. Shikamoo | 2. Alamsiki | 3. Jioni |
| 4. Starehe  | 5. Makiwa   |          |

## **NGELI YA A - WA**

1. Ndovu huyu ni mnene sana .
2. Ni mnyama yupi aliyeharibu mimea?
3. Mbwa wangu siye wako.
4. Mama yangu amefika salama?
5. Ndege ni yule anayeruka angani.

## **NGELI YA KI - VI**

1. Vyoo hivi ni vyao.
2. Vyombo vyenu vimebingirikabingirika.
3. Vyama vyao vilisambaratika.
4. Vichaka vile virefu vina simba wengi.
5. Viini vinavyosababisha UKIMWI vimejulikana.

## **NGELI YA LI - YA**

1. Duka liuzalo manukato limefungwa
2. Shamba lake ni kubwa
3. Gari la janadume hilo ni kubwa
4. Jino hili litang'olewa
5. Shoka lile litanolewa

## **NGELI YA U - I**

1. Maji yamo mitungini
2. Miti iliyokatwa itauzwa bei ghali
3. Mimea ambayo ilingolewa imekauka
4. Miparachichi haitapandwa mashambani
5. Mikebe itakayopatikana itatupwa mashimoni

## **NGELI YA I - ZI**

1. Mimi siandiki barua.
2. Mbavu hazijavunjika.
3. Kucha zake hazitakatwa leo.
4. Ndwele ambazo ziliwapata hazitatibwa.
5. Mwashi hatatengeneza kuta ndefu.

## **NGELI YA U - ZI**

1. Waraka ulioandikwa utatumwa kesho.
2. Wembe wake umepotea.
3. Waya wa sitima uliibwa wiki iliopita.
4. Simba ana ukucha mrefu.
5. Usipoziba ufa utajenga ukuta.

## **VIVUMISHI**

1. Mimi siye wewe wala yeye.
2. Kitabu chako kimeibwa.
3. Ng'ombe wake ameuzwa.
4. Mti wangu utakatwa leo jioni.
5. Wayo wako umedungwa na mwiba.

## **VIASHIRIA RADIDI - VIASHIRIA VISISITIZI**

1. Mikoba ii hii ilinunuliwa jana.
2. Kuimba kuko huko kuliwafurahisha wageni.

3. Wakulima wawa hawa watanufaika na kilimo cha paleto.
4. Matunda yale yale yatapelekwa masokoni.
5. Vyeo vivyo hivyo walivyopandishwa vimevutiliwa mbali.
6. Kuta zizi hizi zilizobomoka zitajengwa upya.
7. Maziwa yayo hayo yameharibika.
8. Wanafunzi wawa hawa wameahidi kutia juhudhi.
9. Ufisadi uo huo ulimitia taabani.
10. Miti iyo hiyo itatumika katika ujenzi.

## **KUBADILISHA SENTENSI KATIKA UMOJA**

1. Uzi uu huu ni wake.
2. Wavu huo huo umekatika.
3. Mkono huu huu umeumia nilipokuwa nikicheza voliboli.
4. Jiwe lile lile litatumika katika ujenzi.
5. Kidonda hicho hicho kitasababisha ugonjwa wa pepopunda.
6. Mwembe huo huo utakatwa asubuhi.
7. Nzi yuyo huyo hueneza kipindupindu.
8. Mahali papa hapa patatumika katika mchezo wa vikapu.
9. Ngozi ile ile ni ya mamba.
10. Ajali hiyo hiyo imesababisha kifo.

## **VIVUMISHI VYA PEKEE**

- |           |            |            |
|-----------|------------|------------|
| 1. yenye  | 2. wenyewe | 3. wote    |
| 4. yoyote | 5. Wenye   | 6. kokote  |
| 7. nyingi | 8. wenyewe | 9. wenyewe |
| 10. wengi |            |            |

## **Vivumishi tasa katika sentensi**

- |              |         |         |
|--------------|---------|---------|
| 1. maridhawa | 2. bora | 3. tele |
| 4. haramu    | 5. duni |         |

## **NYAKATI**

1. Ungefanya bidii ungefaulu.
2. Anapenda kuogelea.
3. Alifika Mombasa jana alfajili.
4. Nitakapoenda kwake sitampata.
5. Wanalima shamba lote leo.
6. Msingetuita tusingiteitika.
7. Nisingalienda kwao juzi nisingalimpata.
8. Wangeishi kwa amani wasinge pigana.
9. Hawakula wala kushiba.
10. Ulisoma kwa bidii na ulifaulu.

## **Usemi halisi na usemi wa taarifa**

1. Joshwa alisema kuwa angeenda kwake jioni hiyo
2. Julius alitaka kujua ninavyoitwa.
3. "Nikiwa tajiri nitanunua gari", Zakaria alisema
4. "Ulikuwa wapi nilipokuita?" Mwalimu Monyoro aliuliza
5. "Mvua itanyesha leo jioni?" Tereza alisema

## **MAJIBU YA KISWAHILI**

### **Udogo na ukubwa wa maneno**

6. Mtoto huyu ana tabia mbaya - watoto hawa wana tabia mbaya.  
Kitoto hiki kina tabia mbaya - vitoto hivi vina tabia mbaya.  
Toto hili lina tabia mbaya - matoto haya yana tabia mbaya.
7. Ng'ombe wangu amevunjika mguu - ng'ombe wetu wamevunjika miguu.  
Kigombe changu kimevunjika kiguu - vigombe vyetu vimevunjika viguu.  
Gombe langu limevunjika guu - magombe yetu yamevunjika maguu.
3. Dawati lake limevunjikavunjika - madati yao yamevunjikavunjika.

Kijidawati chake kimevunjikavunjika - vijidawati vyao vimevunjikavunjika.

Jidawati lake limevunjikavunjika - majidawati yao yamevunjikavunjika.

4. Mwanamke alitishwa na nyoka mtoni - wanawake walitishwa na nyoka mitoni.  
Kijanajike kilitishwa na kijoka kijitoni - vijanajike vilitishwa na vijoka vijitoni.  
Janajike lilitishwa na joka jitoni - majanajike yalitishwa na majoka majitoni.
5. Jiji hili ni kubwa kuliko lolote - majiji haya ni makubwa kuliko yoyote.  
Kijiji hiki ni kikubwa kuliko chochote - vijiji hivi ni vikubwa kuliko vyovyote.  
Mji huu ni mkubwa kuliko wowote - miji hii ni mikubwa kuliko yoyote.